NICOL

*The Economic Shield of the Nation*

**National Investments PLC**
**50 Mirambo Street**
**3rd Floor, Mirambo House**
**P.O. Box 7465**
**Dar Es Salaam**
**Phone: +255 22 2111399/0733006177**
**WhatsApp- 0682 720 679**
**E-mail: invest@nicol.co.tz**

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU MAALUMU KWA WANAHISA WA NATIONAL INVESTMENTS PLC (NICOL)

Taarifa inatolewa tena kwamba Mkutano Mkuu Maalumu wa Wanahisa wa National Investments PLC (NICOL) utafanyika siku ya Jumamosi tarehe **14 Mei, 2022 saa 4.00 asubuhi** katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) Dar es Salaam, Ukumbi wa New Mwanza Hotel jijini Mwanza na Ukumbi wa The Arusha Hotel jijini Arusha. Mkutano huu utafanyika pia kwa njia ya mtandao. Usajili wa Wanahisa utaanza saa 2:00 asubuhi.

**Agenda ya Mkutano Itakuwa Maalumu Kuteua Wakurugenzi wa Bodi ya National Investments PLC (NICOL)**

SOLOMON Stockbrokers

**MAELEZO MUHIMU:**

i. Mwanahisa anaetarajia kuhudhuria mkutano ni lazima kuwasilisha nyaraka zifuatazo: Nakala ya cheti cha Hisa (Depository Receipt) pamoja na Kitambulisho cha Taifa au kitambulisho cha kupiga kura au pasipoti.

ii. Mwanahisa yeyote anayestahili kuhudhuria na kupiga kura, ikiwa hawezi kuhudhuria kwa sababu yoyote ile, anayo haki ya kuteua muwakilishi kuhudhuria, kuzungumza, na, katika kura ya maoni, kupiga kura kwa niaba yake. Muwakilishi huyo si lazima awe mwanahisa wa Kampuni.

iii. Fomu za uwakilishi zitapatikana katika ofisi ya NICOL au kwa kutembelea tovuti ya NICOL www.nicol.co.tz. Fomu za uwakilishi zinapaswa kutumwa ili kufikia ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni au ofisi ya Katibu wa Kampuni au zinaweza kutumwa kwa njia ya barua pepe invest@nicol.co.tz, au kwa njia ya WhatsApp 0682 720 679 kabla ya tarehe 13 Mei 2022.

iv. Wanahisa wanaotaka kuhudhuria mkutano kwa njia ya mtandao wanashauriwa kujiandikisha/ kujisajili mapema mtandaoni kabla ya mkutano kuanza. Maelezo ya kuingia kwenye mtandao yatatumwa kupitia simu yako ya mkononi.

v. Tarehe ya Kufungwa Daftari la Wanahisa wanaostahili kushiriki mkutano itakuwa Alhamisi tarehe 12 Mei 2022.

**KWA IDHINI YA WAKURUGENZI**

__________________________

**Adv. Benjamin Mwakagamba**
**Katibu wa Kampuni**
**April 5, 2022**